

TAARIFA YA IDARA YA KILIMO KATA YA NANJOTA

1. UTANGULIZI

Kata ya Nanjota ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, umbali wa kilomita 11 kutoka Masasi mjini.

Kata ya Nanjota ina jumla ya eneo lenye ukubwa wa hekta 10,585.6, na linalofaa kwa kilimo ni hekta 9,527.1 na eneo linalotumika kwa sasa ni hekta 8,574 ambalo ni sawa na asilimia 90.

2. UZALISHAJI WA KOROSHO NA UFUTA

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, wakulima wa kata ya Nanjota wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na chakula ambapo mazao makuu ya chakula ni muhogo na mahindi, wakati mazao makuu ya biashara ni ufuta, korosho, mbaazi, choroko na alizeti.

Kata ya Nanjota ina jumla ya mikorosho 100,595 ambapo kati ya hiyo midogo ni 13,640, ya umri wa kati ni 37,238 na mikorosho iliyozeeka 49,717 ambapo wastani wa uza;ishaji kwa mikorosho ni chini ya kilo 10 kwa mti mmoja.

Uzalishaji wa korosho na ufuta kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:

Mwaka	Korosho (Tani)	Ufuta (Tani)
2017/2018	849.93	-
2018/2019	641	-
2019/2020	975	-
2020/2021	536	-

3. KAMPENI ONDOA MAPORI ONGEZA UZALISHAJI

Katika kuhakikisha kampeni inatekelezwa na kuleta mafanikio ekari **32** za mikorosho zitaboreshwa kwa kukata mikorosho iliyozeeka, yenye uzalishaji mdogo, iliyopandwa bila kufuata nafasi na kupanda mikorosho sehemu za wazi. Hapa tulipo kwenye shamba la mkulima **Salumu Chande** ambaye ni miongoni mwa wakulima wanaotekeleza kampeni hii. Aidha mkulima huyu amezalisha miche 1200 ya mikorosho bora kutoka TARI Naliendele kwa ajili ya

kupanda sehemu zenye nafasi. Kazi zitakayofanyika katika shamba hili ni pamoja na kukata mikorosho iliyozeeka, kupogolea na kujaza nafasi zilizowazi.

MWISHO

Mwisho natoe shukrani za dhati kwako Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kututembelea ili kuona shughuli zinazofanyika katika maeneo yetu na kuamsha ari kwa wakulima katika shughuli za kiuchumi na hatimaye kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Naomba kuwasilisha.

AFISA KOROSHO